OFISI YA RAIS – TAMISEMI

HALMASHAURI YA WILAYA YA ROMBO

SHULE YA SEKONDARI MAKALEMA

S. L.P 413 Mkuu-Rombo

BARUA PEPE: *makalemasecondary804@gmail.com*

MOB: 0757-185504 or 0768314299

TAREHE: .....

KUMB Na. MDSS/ F1 ..... / .....

JINA LA MWANAFUNZI: .....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKALEMA ILIYOPO WILAYA YA ROMBO MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2021

1.0: UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **Kwanza (I)** katika shule ya **Sekondari Makalema** mwaka 2021

Muhula wa kwanza unaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **22/01/2021**. Soma kwa umakini maelekezo yafuatayo na kuyaelewa vyema:-

2.0: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Shule ipo Tarafa ya Mengwe, Kata ya Mengwe, Kijiji cha Mengwe juu na Kitongoji cha Ng`anyeni. Kibao cha shule kipo barabara kuu itokayo Mwika kuelekea Rombo Mkuu mkabala na Parokia ya Mengwe. Umbali kutoka kibao cha shule hadi shuleni ni Kilometa Moja na Nusu (1.5km) kuelekea barabara ya Ngoyoni Hospitali.

2.1: SARE ZA SHULE

a) Suruali na Sketi mbili (02) zenye rangi ya kitambaa kitakacho ambatanishwa pamoja na fomu ya kujiunga na shule.
b) Mashati mawili (02) ya Tetron meupe ya mikono mifupi, yasiobana na yenye mfuko mmoja.
c) Tai mbili (02) za rangi ya suruali au sketi.
d) Viatu vyeusi vya ngozi, vyenye kamba, kisigino kifupi bapa na visivyochongoka mbele.
e) Soski nyeupe ndefu za kawaida (Stockings)
f) Mkanda mweusi wa kawaidi wa ngozi usio na maandishi au picha yoyote.
g) T. Shirt za michezo zitapatikana katika duka la shule kwa gharama ya Tsh 12,000/-

NB:

1. Mwanao anatakiwa awe amevaa sare ya shule siku anaporipoti shuleni.
2. Suruali za kubana (modo) au fupi na sketi za kubana ambazo hazitafunika mguu wa mwanafunzi mpaka chini kwenye kiwiko hazitakubaliwa na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mwanao.

2.2 : VIFAA VYA KUJIFUNZIA

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na **Daftari kumi na moja (12)** aina ya **Counter Book Quire 3** au **4** kwa ajili ya masomo yake. Daftari zote zijaladiwe kwa karatasi ya kaki na **SIO MAGAZETI.** Pia anaweza kuweka karatasi la nailoni juu ya jaladio la kaki ili kuboresha zaidi.
(ii) Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na **Kalamu ya wino wa Blue au Nyeusi**, **Penseli**, **Ufuto**, **Mkebe wa Hesabu** na **Rula**.
(iii)Kamusi ya Kiingereza – Kiingereza
(iv)Rimu moja (01) ya karatasi zisizo na mistari (A4 plain paper)
(v) Begi la shule kwa ajili ya kubebea madaftari.

2.3: VIFAA VYA USAFI:

Wanafunzi wote wanapaswa kuja na vifaa vya usafi vifuatavyo:-

(i) Ndoo moja (01) ya maji ndogo (lita 10)
(ii) Fagio moja (01) la Chelewa
(iii)Wasichana waje na fagio moja (01) la kukausha maji (Mopa) na Wavulana waje na brashi ngumu moja (01) ya kusugua sakafu.

2.4: MCHANGO WA CHAKULA NA MAENDELEO YA SHULE

Mchango wa Chakula cha wanafunzi utategemea makubaliano ya vikao vya wazazi wenye wanafunzi shuleni na inatakiwa kulipiwa **Benki** ya **NMB**. Jina la akaunti ni **CHAKULA – MAKALEMA SEKONDARI** na namba ya akaunti ni **40410008031.** Malipo yote yafanyike kabla ya kufungua shule. Risiti ya malipo ya benki inatakiwa kuwasilishwa shuleni tarehe ya kuripoti.

2.5: FOMU MUHIMU ZA KUJAZA NA KUSILISHA SHULENI SIKU YA KURIPOTI.

(i) Fomu ya usajili wa mwanafunzi shuleni na maelekezo ya kujiunga na shule.
(ii) Fomu ya upimaji Afya, ijazwe na Daktari (Mganga) wa Hospitali inayotambuliwa na Serikali na **Risiti** ya malipo iambatanishwe pamoja na Fomu kuthibitisha gharama ya matibabu iliyotumika. **NB. Fomu isiyo na risiti haitapokelewa.**
(iii)Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
(iv)Nakala ya cheti cha kuzaliwa

3.0: SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekibishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, walanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote; na
h) Kutunza mali za umma.
i) Kuwasiliana kwa Lugha ya Kiingereza wakati wote uwapo ndani au nje ya shule isipokuwa tuu katika kipindi cha somo la Kiswahili.
j) Kutotoka nje ya uzio wa shule bila kibali maalumu cha Mkuu wa Shule

3.1: MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito / kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAKALEMA

.....
GERSON F. TEMU
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MAKALEMA
S.L.P. 413
MKUU — ROMBO

MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

MAKALEMA SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

To be completed by a Medical Officer in a Government Hospital in respect of all new entrant to Makalema Secondary School.

FULL NAME: .....

AGE : .....

1) Blood count (red and white) .....
2) Stool examination .....
3) Urine examination .....
4) Eye Test .....
5) Ear Test .....
6) Speech Test .....
7) T.B Test .....
8) STD Test .....
9) Spleen .....
10) Abdomen .....
11) Pregnancy test for girls .....
12) Additional information from any Physical, Mental, Hereditary disease or disabilities:

.....
.....
.....
.....

Treatment after examination : .....
.....
.....

MEDICAL CERTIFICATE:

I certify that the above mentioned student has been thoroughly examined by me and found **FIT / UNFIT** to pursue further education.

Signature .....

Full name .....

Designation and official stamp .....

Date .....

Station .....

Kiambatanisho No. 2

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

SHULE YA SEKONDARI MAKALEMA. S. L. P 413 MKUU- ROMBO

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

A. TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI:

(i) Jina kamili : ..... (Alilofanyia mtihani wa darasa la saba)
(ii) Kidato cha: ..... Mwaka : .....
(iii)Tarehe ya kuzaliwa : ..... Dini yake : .....
(iv)Mahali anapoishi (Kata) ..... (Kijiji) .....
(Kitongoji) .....

Picha ya mwanafunzi

YAH: MKATABA NA KAULI YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE HII

1. **MWANAFUNZI:**

Mimi ..... (jina kamili la Mwanafunzi) ninakiri kuwa nimesoma na kuelewa yote kwenye maelekezo ya kujiunga na shule ya Sekondari Makalema, na nitayazingatia kwa muda wote wa masomo yangu hapa shuleni.

Nitakubali kurekebishwa na walezi endapo nitakwenda kinyume na maelekezo hayo kwani maelekezo hayo ndiyo yatakayonifanya nisome kwa bidii na kufaulu mitihani yote itakayotolewa na shule, wilaya, mkoa, kanda na Taifa.

....
SAHIHI TAREHE

2. **MZAZI / MLEZI**

Mimi ..... (Jina kamili) ambaye ni mzazi / mlezi wa ..... (Jina la mtoto anayejiunga na shule). Ninakiri Kupokea, Kusoma na Kuzielewa taratibu zote zilizoko kwanye maagizo / maelekezo ya kujiunga na Shule ya Sekondari ya Makalema. Iwapo mwanangu atakiuka taratibu hizo nitakuwa tayari kukubali hatua zitakazochukuliwa dhidi yake, ili kumwepushia usumbufu. Nitakamilisha kila mwanzo wa muhula mahitaji yote ya shule ikiwa ni pamoja na mchango wa chakula na ulinzi wa shule.

Picha ya mzazi/mlezi wa kiume

Picha ya mzazi/mlezi wa kike

Jina kamili: ..... Jina kamili :.....

Sahihi : ..... **Sahihi : .....**

Tarehe: ..... Tarehe: .....